# Muhtasari
# Tanzania Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu **2014**

Empowered lives.
Resilient nations.

United Republic of Tanzania

## Mageuzi ya Kiuchumi kwa Maendeleo ya Binadamu



## Muhtasari

# Tanzania
# Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu 2014

## Mageuzi ya Kiuchumi kwa Maendeleo ya Binadamu

UNDP
*Empowered lives.*
*Resilient nations.*

United Republic of Tanzania

ESRF
*Implementing Partner*

Hati ya Kumiliki © 2015

**Kimeandaliwa na**
**Economic and Social Research Foundation (ESRF)**
51 Uporoto Street (Barabara ya Ali Hassan Mwinyi),
Ursino Estates S. L. P 31226, Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: (+255) 22 2926084, 2926085, 2926086, 2926087, 2926088, 2926089, 2926090
Simu ya Mkononi: +255 754 780133, +255 655 780233
Nukushi: +255 22 2926083
Barua pepe: esrf@esrf.or.tz au info@esrf.or.tz
Tovuti: http://www.esrf.or.tz au http://www.thdr.or.tz

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
Ofisi ya Tanzania
182 Mzinga way, Barabara ya Msasani, Oysterbay
S.L.P 9182, Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: (+255) 22 2112576, +255 686 036 436

Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Tanzania:
Simu: +255 686 036 436, +255 686 036 436
Ofisi ya Mkurugenzi wa UNDP nchini Tanzania:
Simu: +255 686 036 475, +255 686 036 475
Barua pepe: registry.tz@undp.org
Tovuti: http://www.tz.undp.org

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Fedha,
S.L.P 9111,
Dar es salaam.
Simu: +255 22 2111174 6
Nukushi: +255 22 2110326
Tovuti: http://www.mof.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutoa sehemu ya chapisho hili, kuhifadhali au kuwasilisha, katika umbo lolote au kwa namna yeyote ile, ki eletroniki, kwa kutumia mitambo, kunakili, kurekodi au vinginevyo, bila idhini ya awali.

ISBN 978-9987-770-02-1

Mchoro katika ukurasa wa mbele umebuniwa na ndugu Haji Chilonga wa
La petitie Galerie, Oysterbay Shopping Centre, Barabara ya Toure, Masaki S.L.P 105160 Dar es Salaam, Tanzania.

Kimesanifiwa na kuchapishwa na Jamana Printers, Tanzania

# Dibaji

Kutolewa kwa Ripoti ya kwanza ya Dunia ya Maendeleo ya Binadamu mwaka 1990, kuliashiria mabadiliko ya fikra kuhusu dhana ya maendeleo. Ripoti hii na zile zilizofuatia, zinazotolewa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita, zimebadili namna nchi nyingi zinavyoshughulikia changamoto za maendeleo. Hivi sasa, nchi nyingi zinatumia utaratibu wa kushughulikia changamoto za maendeleo kwa kuwaona watu kama kiini cha maendeleo hayo. Kuanzia wakati huo, nchi nyingi zimekuwa zikiandaa ripoti za maendeleo ya binadamu za nchi au kanda zao kila baada ya kipindi fulani. Kwa jumla, zaidi ya ripoti 600 za mendeleo ya binadamu za kanda, au nchi, zimezinduliwa na zaidi ya nchi 143. Ripoti hizi ni zana za kimkakati, za ushawishi, zinazoandaliwa kupitia mchakato shirikishi ndani ya nchi na kanda husika katika kushughulikia masuala muhimu na kufafanua vipaumbele vya watu. Ripoti hizi ni chanzo muhimu cha ugunduzi na utungaji wa sera za maendeleo na utekelezaji wake.

Toleo hili la Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya Tanzania ya 2014 ni toleo la kwanza, ambalo mada yake kuu ni ***Mageuzi ya Kiuchumi kwa Maendeleo ya Binadamu.*** Katika muongo uliopita, kumekuwapo na mabadiliko ya kimtazamo kuhusu sera za maendeleo kwa kutozingatia kiwango cha matokeo ya mabadiliko pekee bali mabadiliko ya ubora katika ukuaji wa kiuchumi kama yanavyoelezwa katika dhana ya mageuzi ya kiuchumi. Mageuzi ya kiuchumi, kwa namna ya pekee, ni muhimu kwa Tanzania kwa kuwa, wakati Tanzania inashuhudia kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa kinachovutia, cha zaidi ya asilimia 7 tangu mwaka 2000, ukuaji huu hauendi sambamba na kupungua kwa umasikini wa kipato. Serikali ya Tanzania imedhamiria kupunguza umasikini, kwa kiasi kikubwa, na kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Dhamira hii haihitaji ukuaji wa uchumi endelevu pekee, bali mageuzi makubwa ya kiuchumi yanayohusisha mabadiliko ya msingi ya muundo wa uchumi. Ripoti hii inachambua mageuzi ya kiuchumi ambayo ni muhimu ili kuiwezesha Tanzania kufikia lengo la kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025, kama inavyolengwa na dira ya taifa ya maendeleo mpaka 2025. Ripoti hii ina sura nne na viambatisho vya takwimu. Sura ya kwanza inatoa, kwa ufupi, hali ilivyo ya ukuaji wa maendeleo ya binadamu nchini Tanzania. Sura ya pili inajadili maana ya mageuzi ya kiuchumi na inaonyesha chanzo cha mchakato endelevu wa mageuzi ya ukuaji wa kiuchumi nchini Tanzania. Sura ya tatu inajadili aina ya mageuzi ya kiuchumi tunayohitaji, wakati sura ya nne inatoa hitimisho pamoja na maoni ya namna ya kuyafanya mageuzi ya kiuchumi ili yalete maendeleo ya binadamu. Viambatisho vya takwimu vinatoa picha halisi ya viashiria muhimu vya kijamii na kiuchumi vya maendeleo ya binadamu.

Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu nchini Tanzania ya mwaka 2014 imeandaliwa kwa msaada wa mradi wa Maendeleo ya Binadamu wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa ambao unajumuisha mtandao wa ripoti za dunia, kanda na nchi. Ripoti hii iliandaliwa kwa kuwatumia wataalamu na washauri wa ndani na kupata mrejesho kutoka kwa wadau mbalimbali. Wadau hao walikuwa ni wataalamu na watekelezaji wa sera za maendeleo ikiwa ni pamoja na vyombo mbalimbali vya serikali. Uandaaji wa ripoti hii umehusisha mtandao wa wasomi kutoka katika taasisi za kitaifa za utafiti na vyuo vikuu kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa. Asasi ya tafiti za Kiuchumi na Kijamii (ESRF) ilikuwa mshiriki mkuu katika utekelezaji, ikifanya kazi kwa karibu na taasisi muhimu kama Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, na Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Meneja wa mradi na sekretarieti ya uandaaji wa ripoti hii walifanya kazi za kila siku za uandaaji kwa ushirikiano wa karibu na timu ya wataalamu kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Asasi ya tafiti za Kiuchumi na Kijamii, na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vile vile, kikosi kazi kikubwa zaidi, kilichojumuisha wataalamu 35 kutoka katika taasisi mbalimbali za taifa na wakala za maendeleo, walitoa msaada mkubwa, mrejesho na mwongozo katika kipindi chote cha uandaaji wa ripoti hii. Mchakato wa uandaaji ulihusisha kuwapa wataalamu kazi ya kuandika makala kumi, ambazo zilitoa maudhui muhimu kwa ajili ya uandishi wa ripoti hii. Sambamba na hilo, uandaaji wa ripoti ulihusisha ukusanyaji wa kiwango kikubwa wa taarifa mbalimbali kuhusu maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na kutengeneza majedwali yanayoonyesha viashiria vikuu vya maendeleo ya binadamu, kama ilivyowasilishwa kwenye viambatisho vya kitakwimu.

Tumependa kumshukuru Dkt. Hoseana Lunogelo, Mkurugenzi Mtendaji wa ESRF, kwa kutoa fursa kwa asasi yake kusimamia uandaaji wa ripoti hii. Shukurani maalumu zimwendee Dkt. Tausi Kida, Mkurugenzi wa Programu wa

ESRF na Meneja wa Mradi wa kuandaa ripoti hii, kwa uratibu na msaada wa kiufundi wakati wa mchakato wote wa kuandaa na kutoa ripoti hii. Shukurani za pekee ni kwa Profesa Marc Wuyts wa Taasisi ya Mafunzo ya Kijamii ya Uholanzi[1] kwa mwongozo wake wa kitaaluma alioutoa katika mchakato wote. Zaidi ya hayo, shukurani za pekee ziwafikie timu iliyoandaa ripoti hii kwa umakini wao. Timu hiyo inawajumuisha Dkt. Rodgers Dhliwayo (UNDP), Bwn. Amon Manyama (UNDP), Dkt. Tausi Kida (ESRF), Dkt. Jehovaness Aikaeli (UDSM), Dkt. Kenneth Mdadila (UDSM), Bwn. Ahmed Markbel (NBS), Bwn. Sango Simba (NBS), Bwn Deogratias Mutalemwa (ESRF), Bi. Monica Githaiga (UNESCO) na Prof. Marc Wuyts (ISS). Pia, tungependa kumshukuru Dkt. Amarakoon Bandara – Mshauri wa uchumi wa zamani wa UNDP nchini Tanzania – ambaye amefanya kazi muhimu katika hatua za awali za maandalizi ya ripoti hii kabla ya kuhamishiwa katika ofisi za UNDP nchini Zimbabwe.

Shukurani zetu pia ziwafikie timu ya waandaji wa mswada wa ripoti iliyojumuisha wataalamu wafuatao: Dkt. Tausi Kida na Prof. Haidari Amani (sura ya 1); Dkt. Hazel Gray (sura ya 2); Prof. Gelase Mutahaba, Prof. Ernest Mallya na Dkt. Jehovaness Aikaeli (sura ya 3); Prof. Gelase Mutahaba, Prof. Ernest Mallya na Prof. Haidari Amani (sura ya 4), and Dkt. Kenneth Mdadila na Dkt. John Mduma (viambatisho vya takwimu). Uandaaji wa viambatisho vya takwimu ulifanikiwa sana kutokana na msaada mkubwa kutoka katika Ofisi za Taifa za Takwimu za Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa msingi huo, tunalazimika kuwashukuru Dkt. Albina Chuwa – Mkurugenzi Mkuu NBS – na Bwn. Mohamed Hafidh – Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – kwa msada wao katika uandaaji wa ripoti hii ya mwaka 2014. Tunamshukuru Dkt. Richard Whitehead – Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Uhariri na Uchapishaji iliyopo Bergen Norway – kwa kuhariri mswada wa mwisho wa ripoti hii. Tungependa kutoa shukurani zetu kwa Bwn. Nicolai Schulz kwa mchango wake katika uandaaji wa muhtasari wa ripoti na Bwn. Rashid Chuachua kwa kutafsiri muhtasari wa ripoti katika lugha ya Kiswahili. Shukurani maalumu zimfikie msanii wa Kitazania, Bwn. Haji Chilonga, kwa usanifu wa jalada la ripoti hii. Pia, tungependa kumshukuru Bi. Margareth Nzuki na timu nzima ya Idara ya Mawasiliano na Maarifa ya ESRF kwa msada wao wakati wa usambazaji wa ripoti hii. Mwisho, tunamshukuru Bwn. Danford Sango (ESRF) na Bwn. Yasser Manu (ESRF) kwa mchango wao katika uandaaji wa ripoti hii; watu hawa ambao wanaunda sekretarieti ya mradi wa THDR, wametoa mchango mkubwa katika kuratibu shughuli za siku hadi siku katika kipindi chote cha uandaaji wa ripoti hii.

Tungependa kuwashukuru waandishi wafuatao wa makala za utangulizi wa ripoti hii:

(i) Dkt. Tausi Kida na Prof. Haidari Amani – waandishi wa makala ya utangulizi # 1, “Hali na ukuaji wa maendeleo ya binadamu nchini Tanzania”;

(ii) Prof. Marc Wuyts na Dkt. Blandina Kilama – waandishi wa makala ya utangulizi # 2, “Mageuzi ya Kiuchumi nchini Tanzania: Suala la manufaa au matatizo?”;

(iii) Prof. Marc Wuyts na Dkt. Blandina Kilama – waandishi wa makala ya utangulizi # 3, “Mabadiliko ya Uchumi wa Tanzania: mitindo ya ulimbikizaji na mabadiliko ya kimuundo”;

(iv) Dkt. Amarakoon Bandara, Prof. Rajeev Dehejia na Bwn. Shaheen Lavie-Rouse – waandishi wa makala ya utangulizi # 4, “Kiungo kati ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya binadamu”;

(v) Prof. Longinus Rutasitara na Dkt. Jehovaness Aikaeli – waandishi wa makala ya utangulizi # 5, “Utaratibu upi unahitajika ili kufikia lengo la Dira ya Maendeleo ya Tanzania la 2025?”

(vi) Dkt. Razack Lokina na Prof. Anthony Leiman – waandishi wa makala ya utangulizi # 6, “Usimamizi wa maliasili za madini na gesi kwa ajili ya ukuaji endelevu na maendeleo ya binadamu nchini Tanzania”;

(vii) Prof. Alfred Agwanda na Prof. Haidari Amani – waandishi wa makala ya utangulizi # 7, “Ongezeko la idadi ya watu, muundo na mwenendo wake nchini Tanzania”;

(viii) Prof. Phares Mujinja na Dkt. Tausi Kida – waandishi wa makala ya utangulizi # 8, “Matokeo ya mabadiliko ya sekta ya afya nchini Tanzania: sera, viashiria na upatikanaji wa huduma za afya”;

(ix) Prof. Suleman Sumra and Dkt. Joviter Katabaro – waandishi wa makala ya utangulizi # 9, “Kushuka kwa ubora

1 ISS—Institute of Social Studies

wa elimu nchini Tanzania: mapendekezo ya kukabiliana na mwenendo huu";

(x) Prof. Flora Kessy na Bi. Mashavu Omar – waandishi wa makala ya utangulizi # 10, "Hali halisi ya maendeleo ya binadamu na matarajio ya Zanzibar kuifikia Dira ya Maendeleo 2020".

Maandalizi ya Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2014 yamenufaika kwa kiasi kikubwa kutokana na mrejesho na mwongozo uliotolewa na wajumbe wa kikosi kazi cha kuandaa ripoti, chini ya uenyekiti wa Dkt. Servacius Likwelile – Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Wajumbe wengine walitokea katika ofisi zifuatazo: Wizara ya Fedha, ESRF, NBS, Tume ya Mipango, Ofisi ya Rais, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (OCGS), UDSM, REPOA, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Taasisi ya UONGOZI, Hakielimu, UNDP, Shirika la Kazi Duniani, Benki ya Dunia, Shirika la Afya la Dunia, UNICEF, Bunge la Tanzania, Jukwaa la Utu wa Watoto[2] na Shirika la Kimataifa la Kusaidia Wazee.[3] Tungependa kuwashukuru wajumbe wa kikosi kazi cha uandaaji wa ripoti kwa msaada wao usio na kikomo katika kipindi chote cha uandaaji wa ripoti hii.

Uzinduzi rasmi wa mradi wa kuandaa Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya Tanzania ulifanyika bungeni tarehe 31 Agosti, 2013 na ulihudhuriwa na wabunge zaidi ya 200. Tukio hilo lilitumika kama fursa ya kuomba ushauri kwa wabunge kuhusu mada kuu ya ripoti ya mwaka 2014. Kwa heshima kubwa, tunamshukuru Mh. Shamsi Vuai Nahodha, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wa wakati huo, ambaye alizindua tukio hili kwa niaba ya Mh. Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Serikali ya Tanzania. Tunaishukuru Ofisi ya Bunge, inayoongozwa na Mh. Spika Anne Makinda, kwa ukarimu wake katika kufanikisha mradi wa uandaaji wa ripoti na Mh. Job Ndungai, Naibu wa Spika, kwa kuongoza shughuli ya uzinduzi wa mradi wa THDR. Shukurani maalumu ziwafikie wabunge wote walioshiriki katika sherehe za uzinduzi na kwa michango yao kuhusu mada kuu ya ripoti ya mwaka 2014.

Hatimaye, tunashukuru kwa busara na mwongozo uliotolewa na Mh. Prof. Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa Kongamano la Kitaifa lililoandaliwa na ESRF kuhusu "Kufungua Fursa za Kukuza Uchumi: Mageuzi ya Kiuchumi kwa Maendeleo ya Binadamu, lililofanyika tarehe 11 Septemba, 2014. Mada kuu ya kongamano hilo la kitaifa ilitokana na Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2014, na kongamano lilihusisha uwasilishaji wa mada na majadiliano kuhusu makala kumi za utangulizi. Ni matumaini yetu kuwa ripoti hii itatoa uelewa mpana kuhusu uhusiano kati ya mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu nchini Tanzania — changamoto zake, fursa zake na vikwazo vyake. Zaidi ya hayo, pia tuna matumaini kuwa ripoti itatumika kama zana ya kuchochea uchaguzi mzuri wa sera, kufanya maamuzi sahihi, na hivyo kuleta mabadiliko nchini.

**Dkt. Servacius Likwelile**
Katibu Mkuu,
Wizara ya Fedha,
Tanzania

**Bwn. Alvaro Rodriguez**
Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa na
Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo
la Umoja wa Mataifa,
Tanzania

2 Children's Dignity Forum
3 Help Age International

# Yaliyomo

Dibaji iii
Yaliyomo vi
Orodha ya ramani vi
Orodha ya vielelezo vi
Vifupisho vya maneno vii
Utangulizi viii

Sura ya 1
**Hali ya maendeleo ya binadamu nchini Tanzania 1**
Mambo muhimu ya Maendeleo ya Binadamu 3
Idadi ya Watu na Maendeleo ya Binadamu nchini Tanzania 4

Sura ya 2
**Mageuzi ya kiuchumi yanayoendelea: Kuangalia zaidi ya Ukuaji wa uchumi 5**
Mwanzo wa Mageuzi ya Kimuundo 6
Ajira na Mageuzi ya kiuchumi 8

Sura ya 3
**Ukuaji wa uchumi na maendeleo ya binadamu: Msisitizo katika mabadiliko ya sera za uchumi 10**
Historia ya Sera za Uchumi za Tanzania tangu 1961 10
Masuala muhimu na Vikwazo kwa Mustakabali wa Sera za Uchumi 11

Sura ya 4
**Kuyafanya mageuzi ya kiuchumi yalete maendeleo ya binadamu nchini Tanzania 13**
Mageuzi Muhimu ya Kiuchumi 13
Mambo Muhimu katika Kuhakikisha Uhusiano Wenye Manufaa kati ya Mageuzi ya Kiuchumi na Maendeleo ya Binadamu 15
Ujumbe Mahususi 16

# Orodha ya ramani

Ramani ya 1: Mgawanyo wa mikoa ya Tanzania Bara kulingana na kipimo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI) kitaifa 1
Ramani ya 2: Mikoa ya Tanzania Bara ikioanishwa na kipimo cha HDI cha kimataifa 2

# Orodha ya vielelezo

Kielelezo cha 1: Hali ya Umasikini kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) na Kipimo cha Umasikini kwa kutumia Vigezo mbalimbali (MPI), Tanzania Bara 3
Kielelezo cha 2: Mabadiliko ya pato halisi la Taifa kwa mwaka (kwa silimia) 5
Kielelezo cha 3: Mchango wa kisekta kwenye Pato la Taifa (%) 1998-2012 6
Kielelezo cha 4: Viwango vya ukuaji wa kisekta 1999-2012 6
Kielelezo cha 5: Viwango vya ukuaji wa sekta ndogo za huduma 7
Kielelezo cha 6: Mgawanyo wa ajira katika sekta kuu (%) 8
Kielelezo cha 7: Kiwango cha ongezeko la watu wanaofanya na wasiofanya kazi 14

# Vifupisho vya maneno

| | |
|---|---|
| DFID | Department for International Development |
| ESRF | Economic and Social Research Foundation |
| GDP | Gross Domestic Product |
| HBS | Household Budget Survey |
| HDI | Human Development Index |
| HIPC | Highly Indebted Poor Countries |
| ILFS | Intergrated Labour Force Survey |
| ISS | Institute of Social Studies |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MPI | Multi Dimensional Poverty Index |
| NBS | National Bureau of Statistics |
| OPHDI | Oxford Poverty and Human Development Initiative |
| SUA | Sokoine University of Agriculture |
| THDR | Tanzania Human Development Report |
| UDSM | University of Dar es Salaam |
| UNESCO | United Nations Educational Scientific and Cultural Organization |
| UNICEF | United Nations Children's Fund |
| UNDP | United Nations Development Programme |

# Utangulizi

Katika muongo ulipita, Tanzania imeshuhudia ukuaji mzuri wa Pato la Taifa wa kiwango cha wastani wa asilimia 7. Hata hivyo, kinyume cha matarajio ya wengi, ukuaji huu haukwenda sambamba na kupungua kwa umasikini, isipokuwa kwa maeneo machache, kama vile, kupunguza kiwango cha vifo vya watoto na kuongezeka kwa uandikishwaji wa wanafunzi. Kwa jumla kiwango cha maendeleo ya binadamu nchini Tanzania hakiridhishi. Nchi imeshuka kwa nafasi saba katika vigezo vya maendeleo ya binadamu vya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) vya mwaka 2014. Ukuaji wa kiuchumi umeshindwa kuongeza uwezo wa wananchi walio wengi kuishi maisha bora.

Ripoti hii inaonyesha kuwa ukuaji wa uchumi, japo ni jambo muhimu na linalohitajika lakini halitoshi. Tanzania haipaswi kutilia mkazo matokeo ya jumla pekee katika ukuaji wa uchumi, bali msisitizo uwekwe kwenye mabadiliko ya ubora wa uzalishaji unaokwenda sambamba na mchakato wa ukuaji wa uchumi. Nchi inahitaji mageuzi ya kiuchumi yanayoleta maendeleo ya binadamu. Mageuzi ya kiuchumi maana yake ni mabadiliko ya muundo katika uchumi, yanayoambatana na mchango mdogo kutoka katika sekta ya kilimo na mchango mkubwa kutoka katika sekta ya viwanda na utoaji huduma, vinavyokwenda sambamba na mageuzi katika kupunguza viwango vya uzazi na vifo. Ili mageuzi ya kiuchumi yalete maendeleo ya binadamu, ni muhimu mageuzi hayo yaende sambamba na kutengeneza fursa za ajira, kukuza kipato, pamoja na kuongeza huduma za jamii. Tukiieleza dhana hii kwa namna nyingine, mageuzi ya kiuchumi yenye tija, yanakwenda sambamba na kupungua kwa umasikini kwa kiasi kikubwa na kuboreshwa kwa viwango vya maisha ya binadamu. Utoaji wa huduma bora za jamii, kama vile, afya, elimu, na maji safi ni muhimu katika kuhakikisha ushiriki wa Watanzania katika shughuli za kiuchumi. Kwa mwongozo na uongozi imara wa serikali, pamoja na sekta binafsi, mageuzi ya kiuchumi yanaweza kuongeza uzalishaji, kutengeneza ajira, na kuhakikisha uwepo wa huduma za jamii, na hivyo kuleta maendeleo ya binadamu.

Muhtasari huu unafuata muundo wa ripoti kuu ya Maendeleo ya Binadamu Tanzania ya 2014: Sehemu ya (I) inafanya uchambuzi kuhusu hali ya maendeleo ya binadamu nchini Tanzania na kutoa maelezo kuhusu mabadiliko mawili ya kidemografia ambayo ni muhimu ili kuelewa mageuzi ya kiuchumi. Sehemu ya (II) inatoa ufafanuzi wa kina kuhusu dhana ya mageuzi ya kiuchumi na kuchambua mageuzi ya kiuchumi yanayotokea hivi sasa nchini Tanzania. Inaeleza umuhimu wa sera za kiuchumi kwa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu. Sehemu ya (III) inatoa muhtasari wa historia ya sera na mageuzi ya kiuchumi nchini Tanzania tangu uhuru hadi sasa. Sehemu ya (IV) inapendekeza hatua na sera zinazoweza kufanya mageuzi ya kiuchumi yalete maendeleo ya binadamu nchini Tanzania. Hitimisho linatoa muhtasari wa matokeo ya ripoti na kutoa mapendekezo kupitia maeneo muhimu saba.

# 1.

# Hali ya maendeleo ya binadamu nchini Tanzania


Maendeleo ya binadamu ni dhana inayojulikana sana nchini Tanzania. Tangu mwaka 1973, Rais wa kwanza na Baba wa Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alikwishajenga uelewa kuhusu dhana hii sambamba na fikra za mwanafalsafa maarufu Amartya Sen pamoja na mtazamo wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa kuhusu namna ya kushughulikia maendeleo ya binadamu. Nyerere aliona kwamba kukua kwa uchumi ni moja tu kati ya nyenzo za kuleta maendeleo kwa Watanzania. Baadaye, Sen alisema maendeleo ya binadamu ni mchakato wa kuongeza uwezo wa watu kuishi maisha bora. Nyerere anakubaliana na Sen kwamba msingi wa kuongeza uhuru kwa watu unasisitiza umuhimu wa kuwawezesha watu katika maeneo ya afya, umri wa kuishi, elimu na kipato.

Kwa bahati mbaya, katika miongo ya hivi karibuni, Tanzania haikupata maendeleo kama alivyotamani Baba wa Taifa. Kinyume na shauku kubwa iliyokuwepo mara baada ya uhuru, ya kujenga Taifa lenye maendeleo makubwa ya binadamu, hali ya maendeleo ya binadamu hadi sasa siyo ya kuridhisha. Ushahidi mzuri wa jambo hili ni ule unaotolewa na kipimo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI). Kipimo cha HDI, hupima maendelo ya binadamu katika nchi kwa kuzingatia mkusanyiko wa vigezo vya umri wa kuishi, elimu na kipato, kipimo cha chini huwa ni 0 na cha juu ni 1. Kwa kipimo cha 0.488, Tanzania imeshuka kufikia daraja la chini la nchi zenye kiwango kidogo zaidi cha maendeleo ya binadamu. Ipo nafasi ya 159 kati ya 187 duniani. Ripoti ya UNDP kuhusu Maendeleo ya Binadamu Duniani ya mwaka 2014 imeiweka Tanzania katika kundi la nchi zenye maendeleo ya binadamu ya kiwango cha chini. Kinachoshitusha ni kushuka kwa nafasi saba zaidi katika Kipimo cha HDI, ukilinganisha na mwaka 2013.

Katika ngazi ya mikoa, kipimo cha HDI kinaonyesha tofauti kubwa ya viwango vya maendeleo ya binadamu ndani ya Tanzania. Ramani ya 1 inalinganisha viwango vya kipimo cha HDI katika mikoa ya Tanzania, ambapo mikoa 21 ya Tanzania Bara imepangwa kwenye makundi matatu kulingana na kiwango chake cha maendeleo ya binadamu. Theluthi moja ya mikoa hiyo yenye kiwango cha juu cha maendeleo ya binadamu imeonyeshwa kwa rangi ya kijani, na inajumuisha mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Iringa, Ruvuma, Mbeya, na Tanga. Kundi la pili, ni mikoa yenye kiwango cha kati cha maendeleo ya binadamu inayojumuisha mikoa 7: Mwanza, Mara, Manyara, Morogoro, Rukwa, Mtwara, na Lindi. Kundi la tatu ni mikoa yenye kiwango cha chini kabisa cha maendeleo ya binadamu inayojumuisha Kigoma, Singida, Dodoma, Kagera, Tabora, Shinyanga, na Pwani.

## Ramani ya 1

Mgawanyo wa mikoa ya Tanzania Bara kulingana na kipimo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI) kitaifa




Chanzo: Imetayarisha kwa kutumia takwimu Repoti ya Maendeleo ya Binadamu ya Tanzania, 2014

Ramani ya 2, inaonyesha mikoa 21 ya Tanzania Bara kwa kuoanisha na kiwango cha kipimo cha HDI cha kimataifa. Kwa maneno mengine, ramani hii inaonyesha kiwango cha maendeleo ya binadamu kwa ulinganisho kati ya mikoa ya Tanzania Bara na nchi zingine duniani. Ripoti za maendeleo ya binadamu duniani kwa kawaida huzipanga nchi katika makundi manne kama ifuatavyo:

(i) Maendeleo ya binadamu ya juu sana, kundi la 1: 0.955–0.805 (nchi 49),

(ii) Maendeleo ya binadamu ya juu, kundi la 2: 0.796–0.712 (nchi 53),


(iii) Maendeleo ya binadamu ya Kati, kundi la 3: 0.796–0.712 (nchi 42),

(iv) Maendeleo ya binadamu ya chini, kundi la 4: 0.796–0.712 (nchi 43),

Ramani ya 2 inaonyesha kwamba katika makundi haya ya kidunia, hakuna hata mkoa mmoja wa Tanzania unaoweza kulinganishwa na makundi ya kwanza ya kiwango cha maendeleo ya binadamu, yaani kundi la maendeleo ya juu sana ya binadamu na lile la maendeleo ya juu ya binadamu. Kama ramani inavyoonyesha, ni mikoa mitatu tu, yaani Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam ndiyo yenye viwango vinavyoweza kulinganishwa na nchi za viwango vya kati duniani. Mbali na mikoa hii mitatu, mikoa mingine yote ina viwango sawa na nchi zenye kiwango cha chini cha maendeleo ya binadamu.

## Ramani ya 2

Mikoa ya Tanzania Bara ikioanishwa na kipimo cha HDI cha kimataifa





Chanzo: Imetayarisha kwa kutumia takwimu Repoti ya Maendeleo ya Binadamu ya Tanzania, 2014

Kushuka kwa nafasi ya maendeleo ya binadamu nchini Tanzania, kumethibitishwa pia na Kipimo cha Umaskini kwa Kutumia Vigezo Mbalimbali (MPI). Kipimo cha umaskini cha MPI ni kipimo cha maendeleo ya binadamu ambacho hupima kwa mapana ukosefu wa mahitaji muhimu kwa watu na kaya zao. Katika miaka ya karibuni, Kipimo cha umaskini cha MPI kimekuwa ni mbinu mbadala katika kupima kiwango cha umasikini. Katika ripoti ya maendeleo ya binadamu duniani ya mwaka 2013, kwa mfano, hali ya umasikini kwa nchi mbalimbali imewasilishwa kwa kuzingatia viwango vya Kipimo cha Umasikini kwa kutumia MPI. Katika ripoti hiyo, Kipimo cha Umasikini cha MPI kilitumika kwa majaribio na kiliandaliwa na asasi inayopambana na umasikini na kutetea maendeleo ya binadamu ya Oxford (OPHDI). Hata hivyo, katika ripoti ya maendeleo ya binadamu duniani ya mwaka 2014, Kipimo cha Umasikini cha MPI hakikutumika kama kipimo cha majaribio tu bali ni kipimo cha msingi cha kupimia hali ya maisha. Jambo la msingi kwa upande wa Kipimo cha MPI ni kwamba kinatupatia njia mbadala ya kupimia kiwango cha umaskini— yaani, kwa kutumia njia ya kipato cha mtu mmojammoja (headcount).

Kielelezo cha 1 kinaonyesha ukubwa wa tofauti kati ya vipimo vya umaskini. Wakati Kipimo cha Umasikini cha MPI kimeonyesha kuwa asilimia 64 ya Watanzania Bara ni masikini na asilimia 31.3 wanaishi katika hali ya umasikini uliokithiri, kipimo cha umasikini kwa kigezo cha kipato kwa mtu mmoja mmoja kutokana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) unakadiria kuwa viwango ya umasikini ni asilimia 28.2 na umasikini uliokithiri asilimia 9.7 tu. Ingawa kuna tofauti kubwa, vipimo vyote vinaashiria mambo mawili: viwango vya umasikini ni vikubwa na Lengo la Maendeleo la Milenia la kufikia kiwango cha umasikini cha asilimia 18 hadi 2015 haliwezi kufikiwa.

## Kielelezo cha 1

Hali ya Umasikini kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) na Kipimo cha Umasikini kwa




Chanzo: THDR 2014; kipimo MPI kutumia TDHS 2010 na HBS 2012.

## Funguo

1. Umaskini wa kipato kwa kuhesabu mtu mmoja mmoja, Utafiti wa Mapato na Matumizi kwa Kaya 2012 (Poverty headcount, HBS 2012),
2. Umaskini uliokithiri, Utafiti wa Mapato na Matumizi kwa Kaya 2012 (Extreme Poverty, HBS 2012),
3. Umaskini kwa kuhesabu mtu mmoja mmoja, Kipimo cha Umaskini kwa kutumia Vigezo mbalimbali 2013 (Poverty headcount, MPI 2013)
4. Umaskini wa uliokithiri kwa kutumia Vigezo mbalimbali 2013 (Extreme Poverty, MPI 2013)

## Mambo muhimu ya Maendeleo ya Binadamu

Ili kufanya uchambuzi wa kina kuhusu hali ya maendeleo ya binadamu nchini Tanzania, ripoti inaangalia kwa undani vipengele tofauti vya Kipimo cha HDI na Kipimo cha umaskini cha MPI. Licha ya Ongezeko la Pato la Taifa kwa kiwango cha asilimia 7 katika muongo uliopita, kiwango cha umaskini kimepungua kidogo sana kutoka asilimia 33.3 mwaka 2007 hadi asilimia 28.2 mwaka 2012.[4]

Picha halisi ya umaskini nchini Tanzania inathibitishwa na hali ya umaskini inayoonyesha viwango vya chini vya

4 Kwa mujibu wa kipimo cha umasikini kwa kigezo cha kipato kwa mtu mmojammoja kutokana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya.

maisha katika kaya nyingi. Pamoja na hilo, ni ukweli unaojulikana sana kuwa umaskini nchini Tanzania umekithiri huko vijijini ambapo viwango vya maisha ni vya chini ukilinganisha na kaya za mijini. Kwa mfano, wakati utumiaji wa umeme kwa ajili ya mwanga umeongezeka mara mbili kutoka asilimia 10 mwaka 2002 hadi asilimia 21 mwaka 2012, matumizi katika maeneo ya vijijini ni asilimia 8 (ukilinganisha na asilimia 49 katika maeneo ya mijini). Zaidi ya hayo, asilimia 67 ya kaya nchini Tanzania zinaishi katika makazi yenye sakafu za udongo, mchanga au kinyesi cha ng'ombe, wakati asilimia 63 hazina fursa ya kupata maji ya bomba kama chanzo kikuu cha maji ya kunywa. Vilevile, matumizi ya kuni kama nishati ya kupikia na ukosefu wa huduma za usafi kwa watu walio wengi bado ni tatizo.

Kuhusiana na afya, Tanzania imepiga hatua kubwa katika muongo uliopita. Umri wa wastani wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 51 mwaka 2002 hadi 61 mwaka 2012. Vifo vya watoto vimepungua kutoka vifo 68 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa mwaka 2002 hadi kufikia vifo 45 mwaka 2010. Hivyo, Lengo la Milenia la kupunguza vifo vya watoto hadi kufikia watoto 38 kwa kila 1000 wanaozaliwa ifikapo mwaka 2015 linaonyesha uwezekano wa kufikiwa. Hata hivyo, utapiamlo unaonekana kuwa miongoni mwa tishio kubwa kwa maendeleo ya binadamu nchini Tanzania. Upatikanaji wa vyakula muhimu na vyenye virutubisho vya kutosha[5] haujaongezeka tangu mwaka 1997, na utapiamlo uliokithiri unakadiriwa kuwa ni sababu kubwa ya zaidi ya theluthi ya vifo vya watoto chini ya umri wa miaka 5.

Hali ya elimu nchini Tanzania inakanganya; Kwa upande wa mafanikio, tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000 sekta ya elimu imeshuhudia maendeleo ya kuridhisha kwa upande wa uandikishaji wanafunzi kwa ngazi zote. Kwa mfano, asilimia 80 ya watoto wenye umri wa kwenda shule, kwa sasa wapo shuleni (miaka 7—13). Kwa upande wa matatizo, ubora wa elimu inayotolewa nchini Tanzania ni wa kiwango cha chini. Zaidi ya hayo, sekta ya elimu nchini inakabiliwa na ongezeko la wanafunzi wanaoacha shule, umahiri mdogo na kukosekana kwa ari na motisha kwa walimu. Ijapokuwa umma ulioelimishwa vema ni kichocheo cha mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu, ubora wa elimu nchini Tanzania hauridhishi.

## Idadi ya Watu na Maendeleo ya Binadamu nchini Tanzania

Hatimaye, ni muhimu kuzingatia namna mbili za mabadiliko maalumu ya kidemografia: ongezeko la idadi ya watu na ukuaji wa miji. Ingawa sio vigezo vya moja kwa moja vya maendeleo ya binadamu, vina mchango mkubwa kwa maendeleo ya binadamu na mageuzi ya kiuchumi. Kutegemeana na kasi ya mambo hayo mapito ya "mzunguko wa maisha ya binadamu"—yaani uzazi, ndoa, uhamaji, na vifo—vinaweza kutengeneza fursa na changamoto tofauti tofauti za kiuchumi na kimazingira.

Kutokana na ongezeko la watu la asilimia 2.7 kwa mwaka, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi zenye ongezeko la haraka sana la idadi ya watu. Kwa kuwa na ongezeko la watu milioni 1.2 kwa mwaka, inaonyesha kuwa idadi kubwa ya watu ni vijana. Kuwa na idadi kubwa ya vijana kunaweza kuwa kikwazo na pia fursa kwa Tanzania. Kwa kuwa na kiwango duni cha elimu na fursa finyu za ajira, Tanzania itashuhudia ongezeko kubwa la vijana wasio na elimu ya kutosha na ajira. Hata hivyo, iwapo Tanzania itafanikiwa kuboresha elimu yake na kutengeneza fursa za ajira, inaweza – kama ilivyofanya China katika miongo mitatu iliyopita—kuwa na vijana wenye kiwango cha chini cha utegemezi ambao watakuwa na ari na sifa zinazotakiwa ili kuajiriwa.

Namna ya pili ya kuuelezea mwelekeo wa kidemografia nchini Tanzania ni ukuaji wa miji, yaani kuongezeka kwa idadi ya watu mijini ikilinganishwa na maeneo ya vijijini Tangu uhuru, Tanzania imeshuhudia ongezeko kubwa la idadi ya watu mijini. Kwa sasa, idadi ya watu katika miji inaongezeka kwa kiwango cha karibu asilimia 5 kwa mwaka. Kama ilivyo kwa upande wa ongezeko la idadi ya watu, ukuaji wa miji una faida na madhara yake kwa maendeleo ya binadamu. Kwa upande mmoja, ongezeko la watu lisilodhibitiwa katika miji linaweza kusababisha kuwapo kwa makazi holela na kuelemewa kwa uwezo wa miji katika utoaji wa huduma za jamii. Hali inakuwa mbaya zaidi kutokana na tatizo la miji kukosa uwezo wa kutoa fursa za ajira kukidhi mahitaji ya nguvu kazi inayozidi kuongezeka. Kwa upande mwingine, miji wakati wote ni kiini cha maendeleo ya kiuchumi. Ni mahali pa masoko, biashara, makutano ya njia kuu za usafirishaji, vituo vya uwekezaji wa kitaifa na kimataifa, pia ni vituo vya uzalishaji na ubunifu. Kutokana na msongamano mkubwa wa watu katika maeneo ya mijini, serikali zinaweza kuhakikisha upatikanaji wa miudombinu muhimu kwa urahisi na kutoa huduma kwa gharama za chini. Hivyo basi, miji inabaki kuwa kiini cha mageuzi ya kiuchumi, ijapokuwa inakabiliwa na vikwazo kadhaa.

5 Caloric requirements

# 2.


# Mageuzi ya kiuchumi yanayoendelea: Kuangalia zaidi ya ukuaji wa uchumi

Kama ilivyoonyeshwa katika sehemu iliyopita, ukuaji wa uchumi wa Tanzania unaovutia katika muongo uliopita umeshindwa kuleta tija kwa maendeleo ya binadamu. Dhana iliyojengeka kuwa ukuaji wa kiuchumi ungeyafikia makundi yote katika jamii imeshindwa kuthibitika. Ijapokuwa ukuaji wa uchumi ni muhimu, lakini hautoshi kuboresha viwango vya maisha na kupunguza umasikini. Kinachotakiwa ni mabadiliko jumuishi zaidi: mageuzi ya kiuchumi yanayojumuisha sio tu ukuaji wa kiuchumi, bali pia mabadiliko ya msingi ya muundo wa uchumi wenyewe pamoja na kutengeneza fursa za ajira na kuboresha huduma za jamii. Dhana ya mageuzi ya kiuchumi iliibuka katika miaka ya 1950 na 60. Kwa kawaida yanahusu mabadiliko ya kimuundo katika uchumi kutoka kwenye utegemezi wa kilimo na kwenda kwenye viwanda na utoaji huduma. Haya ni lazima yaende sambamba na mabadiliko ya kidemografia kwa kupunguza kiwango cha vizazi na vifo. Mageuzi ya kiuchumi husisitiza umuhimu wa kuongeza thamani katika uzalishaji kunakotokana na mchakato wa ukuaji kiuchumi, kuliko kuzingatia ongezeko la uzalishaji tu.

Hata hivyo, ukuaji wa uchumi na mabadiliko ya kimuundo pekee havitoshelezi kuufanya uchumi ulete maendeleo ya binadamu. Kama itakavyoonyeshwa kwa undani, muundo wa uchumi wa Tanzania umekuwa ukibadilika tangu mwanzoni mwa ulegezaji wa masharti ya kibiashara katikati ya miaka ya 1980— bila ya mabadiliko yoyote makubwa katika maendeleo ya binadamu. Ili kuwezesha maendeleo ya binadamu, mageuzi ya kiuchumi yanatakiwa kuzalisha mali nyingi inayotosheleza mahitaji ya mtu binafsi na ya watu wote kwa kupanua uwezo na uhuru wa binadamu. Wakati ukuaji wa kiuchumi unaongeza kipato, mara nyingi, unashindwa kuwafanya wanajamii wagawane kwa usawa kipato hicho. Sababu kubwa ya jambo hili ni kwamba kukua kwa uzalishaji kulikoshuhudiwa katika viwanda na huduma nchini Tanzania kimsingi kulisukumwa na ongezeko la tija kuliko ongezeko la fursa za ajira. Matokeo yake, ijapokuwa uchumi unakua, watu wengi wanakosa ajira na wengine wanaajiriwa kwa viwango vya chini vya malipo, na hivyo, kushindwa kuboresha maisha yao. Hivyo, kuongeza fursa za ajira na kipato kizuri ni muhimu ili kuwa na mageuzi shirikishi ya kiuchumi na yanayopunguza umasikini. Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, uchumi wa Tanzania umeshapitia mabadiliko makubwa muhimu: viwango vya ukuaji wa uchumi kwa sasa vipo juu na vimeimarika zaidi (angalia kielelezo cha 2); mfumuko wa bei upo chini na uchumi mkubwa umeimarika; matumizi katika ngazi zote yameongezeka; kutokana na kuongezeka kwa mapato ya ndani utegemezi wa misaada toka nje umepungua; kwa jumla, uchumi umekuwa huria na wenye mwingiliano na wa dunia, huku uwekezaji kutoka nje na biashara vikiongezeka. Kwa kuwa mageuzi ya kiuchumi yanategemea mchakato wenye mwelekeo maalumu, tunatakiwa kuchambua namna yalivyotokea katika miaka ya hivi karibuni kabla ya kutoa matarajio au mapendekezo ya baadaye. Kwa hiyo, aya zifuatazo zitafafanua sifa muhimu zilizobainishwa kwa ajili ya mageuzi shirikishi ya kiuchumi nchini Tanzania: mabadiliko ya kimuundo na ajira.

## Kielelezo cha 2

Mabadiliko ya pato halisi la Taifa kwa mwaka (kwa silimia)





Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Mwanzo wa Mageuzi ya Kimuundo

Ukuaji mkubwa na kujumuishwa zaidi katika uchumi wa dunia vimeambatana na mabadiliko katika muundo wa uchumi wa Tanzania. Ingawa kwa kasi ndogo, lakini mabadiliko haya yako sambamba na matarajio mapana ya mageuzi ya kimuundo: mchango wa kilimo katika Pato la Taifa umeshuka kutoka asilimia 29 mwaka 2001 hadi asilimia 24 mwaka 2010, na mchango wa viwanda umeongezeka kutoka asilimia 18 mwaka 2001 hadi asilimia 22.1 mwaka 2012. Sekta ya huduma imeendelea kuongoza katika kuchangia mapato, japo mchango wake ulishuka kidogo kutoka asilimia 45.3 mwaka 2001 hadi asilimia 43.9 mwaka 2012 (tazama Kilelelezo cha 3).

### Kielelezo cha 3

Mchango wa kisekta kwenye Pato la Taifa (%) 1998-2012





Chanzo: Jamhuri ya Muungano ya Tanzania 2007, 2013

Sababu za mabadiliko ya kimuundo ni za aina mbili. Kwa upande mmoja, sekta ya kilimo nchini Tanzania imekua kwa wastani mdogo wa asilimia 4.3 kwa muongo uliopita (tazama Kielelezo cha 4). Hali hii inatokana na ukweli kwamba tija ya kilimo imeendelea kuwa ndogo kwa miaka mingi. Hali kadhalika, mbinu za uzalishaji katika kilimo zimebaki bila kubadilishwa: kilimo bado ni cha wakulima wa mashamba madogo ambacho hutegemea nguvu kazi ya familia. Zaidi ya hayo, matumizi ya teknolojia na pembejeo yamebakia ya kiwango kidogo sana ikilinganishwa na nchi zingine: wakati Tanzania inatumia wastani wa kilo 9 za mbolea kwa hekta, Malawi hutumia kilo 27, na China hutumia hadi kilo 279. Uuzaji nje wa mazao ya kilimo ulikuwa ni sehemu muhimu ya kufanikisha mageuzi ya kiuchumi kwa nchi kama vile Brazil na Vietnam. Nchini Tanzania mchango wa uzalishaji wa mazao ya biashara katika Pato la Taifa ulishuka kutoka asilimia 6.7 mwaka 1996 hadi asilimia 2.8 mwaka 2010. Kwa kuzingatia kwamba bado kilimo kinategemewa moja kwa moja na karibu asilimia 80 ya watu wote, kuboresha viwango vya uzalishaji katika sekta nzima ya kilimo kutakuwa muhimu ili kukuza maendeleo ya binadamu.

### Kielelezo cha 4

Viwango vya ukuaji wa kisekta 1999-2012





Chanzo: Jamhuri ya Muungano ya Tanzania 2007, 2013

Kwa upande mwingine, sekta ya viwanda imekuwa na viwango vya ukuaji vya kuridhisha. Ingawa imezorota katika miaka ya karibuni, katika miaka ya 2003 na 2004 ukuaji wa sekta hiyo ulifikia asilimia 10.9. Wakati hii inaonekana kuwa ishara nzuri kwa mageuzi ya kiuchumi, inapaswa kuzingatiwa kwamba ukuaji wa sekta ya viwanda kimsingi ulisukumwa na upanukaji wa haraka wa sekta ya madini. Kuanzia kwenye kima cha chini kabisa, mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa ulipanda kutoka asilimia 1.8 mwaka 2000 mpaka 3.3 mwaka 2010. Wakati sekta ya madini inabakia pembezoni katika muundo wa jumla wa uchumi, lakini bado umuhimu wake unaongezeka kwa kasi. Sekta ya madini kwa sasa ndiyo mpokeaji mkubwa wa uwekezaji kutoka nje, ikikua kwa wastani wa asilimia 13 katika miaka ya 2000, na inachangia asilimia 40 ya mauzo yote ya nje. Ingawa sekta ya madini ingeweza kutoa mchango mkubwa katika mabadiliko ya uchumi wa Tanzania, mpaka sasa imeshindwa kufanya hivyo kwa sababu kuu nne. Kwanza, uchimbaji rasmi (unaotumia mtaji mkubwa) wa madini una uwezo mdogo tu wa kuajiri watu wengi: Mfano, mwaka 2006, ni asilimia 0.5 tu ya watu waliosema kwamba uuzaji na uchimbaji madini ni ajira yao rasmi na shughuli yao ya msingi ya kiuchumi. Zaidi ya hayo, uchimbaji madini kwa jumla huzalisha mali ghafi na bidhaa chache kwenda kwenye sekta zingine. Tatu, mara nyingi inahusishwa na muundo usio mwafaka na rushwa. Mwisho, kutokana na misamaha ya kodi na labda kutokana na kulipa kodi ndogo, mapato yanayotokana na sekta ya madini ni madogo sana. Kwa mfano, kuanzia mwaka 1998 hadi 2011, wastani wa mapato yaliyozalishwa na sekta ya madini yalichangia asilimia 2.3 tu ya mapato ya ndani. Ingawa uchimbaji usio rasmi ungeweza kuwa na matokeo mapana na ya moja kwa moja kwa mapato ya watu, lakini wenyewe pia unahusishwa na uharibifu wa mazingira, mazingira yenye mashaka na hatarishi ya kazi, pamoja na kuhamishahamisha watu kunakoathiri maendeleo ya binadamu. Mbali na uchimbaji wa madini, sekta ya viwanda inaundwa pia na sekta nyingine mbili ndogo: ujenzi na utengenezaji bidhaa. Zote mbili ni sababu na matokeo ya aina ya ukuaji ulioshuhudiwa nchini Tanzania katika muongo uliopita, sekta ndogo ya ujenzi ilichangia karibu asilimia 35 ya mapato ya sekta ya viwanda katika miaka ya 2000 na ni moja ya sekta zinazokua kwa haraka sana. Licha ya kiwango kikubwa cha ukuaji cha karibu asilimia 9 katika miaka yote ya 2000, sekta ndogo ya utengenezaji bidhaa ndiyo ilikuwa na ukuaji dhaifu zaidi kati ya sekta tatu ndogo za viwanda. Zaidi ya hayo, mchango wake ndani ya Pato la Taifa karibu ulibakia vilevile kwenye asilimia 8 katika miaka yote ya 2000. Kwa kuzingatia kwamba, kihistoria, sekta ya viwanda imekuwa sekta kuu ya kuleta mageuzi ya kiuchumi, kutokukua huku kunasikitisha. Licha ya bei za bidhaa kutokuwa nzuri ukuaji usioridhisha kimsingi ulitokana na sababu mbili. Kwanza, uzalishaji bidhaa umejikita zaidi katika uzalishaji wa bidhaa za aina chache na masoko finyu. Pili uzalishaji mwingi wa bidhaa nchini Tanzania unahusisha uzalishaji wa bidhaa ambazo ni rasilimali, ambazo huongezewa thamani ndogo sana. Sekta ya viwanda inachukua chini ya asilimia 5 ya nguvu kazi, hivyo mchango wake katika kutengeneza nafasi za kazi na kuchochea maendeleo ya binadamu ni mdogo.

Sekta ya huduma ndiyo kubwa zaidi na ambayo inakua kwa uthabiti zaidi katika uchumi wa Tanzania. Ikiwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 8 kati ya mwaka 2001 na 2012, mchango wake umefikia kiasi cha asilimkia 43.9% mwaka 2012. Sekta za mawasiliano na fedha ndizo hasa zimekuwa za kuridhisha, ambapo sekta ya mawasiliano ilikua kwa zaidi ya asilimia 15 tangu mwaka 2003 (Tazama Kielelezo cha 5). Hata hivyo, sekta hizi hulipa mishahara mikubwa na kutoa ajira kwa wenye elimu ya juu tu. Hivyo, mchango wake wa moja kwa moja kwenye kupunguza umaskini ni mdogo. Lakini, sekta nyingine ndogo zenye mchango wa moja kwa moja kwenye maendeleo ya binadamu, kama vile elimu au afya, pia zimekuwa zikikua – ingawa kwa viwango vya chini zaidi.

## Kielelezo cha 5

Viwango vya ukuaji wa sekta ndogo za huduma




Chanzo: Jamhuri ya Muungano ya Tanzania 2007, 2013

## Ajira na Mageuzi ya kiuchumi


Kama ilivyooneshwa hapo juu, mwelekeo na kiwango cha mabadiliko ya ajira katika sekta mbalimbali wakati wa mchakato wa mabadiliko ya kimuundo, vinaongoza aina ya mageuzi ya kiuchumi. Iwapo mabadiliko ya kimuundo yatasababisha wafanyakazi waende zaidi kwenye sekta zenye uzalishaji mkubwa na fursa nyingi za ajira, hapo ukuaji wa uchumi utakuwa wa haraka na jumuishi zaidi, na utatoa mchango mkubwa katika kupunguza umasikini. Ukuaji katika uzalishaji pekee hautaboresha viwango vya maisha mpaka uwe na tija katika kukuza ajira. Ukuaji wa kiuchumi ambao hauna tija katika ajira unasababisha uhitaji wa wafanyakazi wachache. Ili ukuaji katika uzalishaji uboreshe viwango vya maisha, unahitaji uende sambamba na kuongeza fursa za ajira.

Kutokana na ongezeko la haraka la idadi ya watu nchini Tanzania la karibu watu milioni 1.2 kwa mwaka, umuhimu wa kuongeza fursa za ajira unajitokeza. Ukubwa wa nguvu kazi umeongezeka kutoka watu milioni 15.5 mwaka 2001 hadi watu milioni 24.1 mwaka 2012, ikiwa ni kiwango cha asilimia 2.3 kwa mwaka. Hadi sasa, mabadiliko ya kidemografia, yaani kupungua kwa viwango vya vifo na vizazi, ambayo ni sehemu ya mageuzi ya kiuchumi bado hayajafikiwa.

Hata hivyo, licha ya mabadiliko ya kimuundo kwenye mgawanyo wa Pato la Taifa, mgawanyo wa ajira kisekta kwa kiwango kikubwa umebaki bila mabadiliko. Bado, takribani Watanzania asilimia 80 wanafanya kazi katika sekta ya kilimo. Kushuka kulikoonyeshwa katika kielelezo namba 6 kunafafanuliwa kama ubunifu wa kitakwimu, ukielezwa kwa kuondoa watoto kati ya umri wa miaka 10 hadi 14 katika utafiti wa hivi karibuni kuhusu Nguvu Kazi.[6] Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu kwa haraka katika kipindi hicho, mgao huu wa ajira usiobadilika katika sekta ya kilimo, unaakisi kuongezeka kwa kiasi kikubwa kwa watu wanaotegemea kilimo kwa ajira. Kwa sekta zisizo za kilimo, sekta ya viwanda ina mchango mdogo sana katika ajira wa chini ya asilimia 5 ya ajira zote. Sekta ya utoaji huduma ina mchango wa karibu asilimia 15 za ajira. Asilimia 79 ya ajira katika sekta ya utoaji huduma ni ajira zisizo rasmi – zikiwa na mwelekeo wa kupanda.

### Kielelezo cha 6

Mgawanyo wa ajira katika sekta kuu (%)




Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Taifa 1991, 2001, 2006.

Kuhusiana na suala la ajira, ipo mielekeo hasi inayobainika nchini Tanzania. Kwanza, kumekuwa na ongezeko kubwa zaidi la ukuajia wa ajira katika sekta ya kilimo kutoka katika sekta za viwanda na huduma. Pili, ukubwa wa sekta isiyo rasmi katika maeneo ya vijijini na mijini umeongezeka sana, ukikuwa kwa asilimia 105 kati ya mwaka 2000

6 ILFS— Intergrated Labour Force Survey.

na 2006. Hivyo, kinyume na matarajio na mahitaji ya mageuzi ya kiuchumi yenye mafanikio, nguvu kazi ilihama kutoka kwenye shughuli zenye tija zaidi kuelekea kwenye shughuli zenye tija ndogo. Kimsingi, hili linaeleza ni kwa nini ukuaji mkubwa wa uchumi unaweza kwenda sambamba na upunguaji mdogo wa umaskini: ukuaji ulijikita zaidi kwenye shughuli zenye tija kubwa lakini wenye fursa chache za ajira. Matokeo yake, watu wengi walilazimika kuingia kwenye kazi duni katika sekta ya kilimo na ile isiyo rasmi.

Ripoti hii inajenga hoja kwamba sifa kuu mbili za uchumi wa Tanzania zinaweza kuwa ni sababu za kutokea kwa ongezeko la ukosefu wa ajira. Kwa upande mmoja, upanuzi wa sekta rasmi ya viwanda nchini Tanzania haujazalisha ajira mpya za kutosha. Makampuni mapya yaliyoanzishwa tangu mwaka 2005 yamechangia asilimia 11 ya ajira zote za viwandani, hii inaonesha kwamba makampuni hayo yalijikita zaidi katika shughuli ambazo hazikuchangia sana ukuzaji wa ajira. Hata hivyo, kama inavyoonekana katika nchi nyingi za Asia, viwango vya juu vya utengenezaji wa fursa za ajira katika viwanda ndiyo sababu ya ukuaji wa mapato uliokuwa na tija kubwa katika kupunguza umaskini. Pili, ukweli kwamba bei za vyakula zilipanda haraka zaidi kuliko bei zisizo za vyakula, katika miaka ya 2000, ulikuwa na athari kubwa katika ajira. Sio tu kwamba masikini waliathiriwa moja kwa moja na kupanda kwa gharama za maisha, lakini uwezekano wa uzalishaji unaohitaji nguvu kazi kubwa nje ya sekta ya kilimo ulishuka sana kutokana na kupanda kwa ujira.

# 3.

# Ukuaji wa uchumi na maendeleo ya binadamu: Msisitizo katika mabadiliko ya sera za uchumi

Uchambuzi wa mageuzi ya sasa ya uchumi wa Tanzania umeonyesha kwamba bila ya kuongeza fursa za ajira na uhakika wa kujikimu, mageuzi ya kiuchumi yanashindwa kuchochea maendeleo ya binadamu. Ripoti hii inaonyesha kwamba kuunganisha masuala yote mawili kunahitaji hatua za makusudi katika uamuzi wa kisera na utekelezaji wa mikakati. Uhusiano muhimu baina ya mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu unaweza kuonekana kwa utoaji wa elimu na huduma bora za afya. Sio tu kwamba ukuaji bora wa uchumi unahitaji raia wenye afya na elimu bora, lakini upatikanaji wa elimu kwa wote ni njia bora ya kuhakikisha upatikanaji wa kazi na kupitia hilo, uhuru na uwezeshaji wa kiuchumi kwa watu wote utawezekana. Pamoja na hili, nchi ambazo zimeimarisha uhusiano kikamilifu kati ya mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu kwa kutumia sera za kijamii – kama vile Japani, Korea ya Kusini, au Singapore – zimekuwa zikipiga hatua kubwa ya ukuaji wa kiuchumi unaokwenda sambamba na maendeleo makubwa ya binadamu. Ili kuhusianisha mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu, ni muhimu kuongeza matumizi katika sekta hizi.

Licha ya kuwekeza katika elimu na afya, sera nyingine za serikali ni muhimu sana katika kutengeneza mazingira yanayowezesha maendeleo ya binadamu. Kama ilivyosisitizwa awali, serikali inapaswa kutekeleza sera zake katika kutengeneza fursa za ajira, pamoja na kusimamia mgawanyo wa rasilimali za Tanzania. Zaidi ya hayo, inapaswa kutoa fursa ya upatikanaji mkubwa wa rasilimali kwa ajili ya uzalishaji kama vile ardhi, mikopo na miundombinu mwafaka. Mwisho, usimamizi unapaswa kuwa bora zaidi, ukiwamo ushiriki mpana wa wananchi na asasi za kiraia.

## Historia ya Sera za Uchumi za Tanzania tangu 1961

Kama ilivyoelezwa hapo juu, sera ya serikali inaweza kuwa na athari kubwa kwa muundo na mafanikio ya mageuzi ya kiuchumi ndani ya nchi. Ili kujenga uelewa kuhusu mageuzi ya sasa ya kiuchumi na namna ya kuangalia mustakabali wake, tunapaswa kuchambua historia na mabadiliko ya sera na mkakati wa kiuchumi wa Tanzania. Vipindi vitatu ni muhimu sana: tangu uhuru hadi mgogoro wa kiuchumi (1961 hadi 1985), mageuzi ya muundo wa kiuchumi (1986 hadi 2000), na kipindi cha sasa cha upunguzaji umasikini (tangu 2000).

Rais wa kwanza wa Tanzania, Julius K. Nyerere, alikuwa ni mtu muhimu sana katika kufafanua sera ya uchumi wa Tanzania baada ya uhuru. Kama mtetezi mkubwa wa "Ujamaa," serikali yake iliongoza nchi kwa kuwa na mipango ya miaka mitatu na mitano ya uchumi, ambayo kwa kiwango kikubwa au kidogo ilitekeleza itikadi hii. Miongoni mwa nguzo za ujamaa zilikuwa ni kuzingatia kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi, utaifishaji wa njia kuu za uzalishaji mali, elimu ya kujitegemea, kuingiza bidhaa za msingi tu kutoka nje ili kuwezesha uzalishaji wa viwanda vya ndani, na chama kushika hatamu. Zaidi ya hayo, sambamba na mtazamo wa mwanafalsafa Sen na mtazamo wa UNDP kuhusu maendeleo ya binadamu, ujamaa ulikuwa na lengo la kupanua uchaguzi na uhuru wa watu kuishi maisha marefu na yenye afya, kupata elimu na maarifa, na kushiriki katika jamii zao kwa utu na heshima.

Licha ya malengo mazuri na baadhi ya mafanikio katika maendeleo ya binadamu, ujamaa ulikabiliana na vikwazo na udhaifu mwingi. Kutokana na hali ya chama kushika hatamu, miradi mara nyingi ilishindwa kutekelezwa kutokana na fursa ndogo kwa walengwa halisi kushiriki katika utekelezaji. Mkakati wa maendeleo vijijini wa Nyerere wa kiugatuaji madaraka, hasusan, ule wa operesheni vijiji, ulitibua mifumo ya uzalishaji katika kilimo na kustawisha urasimu, ambao zaidi ulinyonya rasilimali katika sekta hiyo. Matokeo yake, watu wengi katika maeneo ya vijijini waliishia kwenye kilimo cha kujikimu, wakajikita kwa kiasi kidogo katika uzalishaji wa mazao ya biashara. Sambamba na ugatuzi huu wa kiuchumi, maendeleo ya binadamu na imani ya wananchi dhidi ya uwezo wa serikali vilipungua. Utumiaji wa nguvu ili kuwarudisha nyumbani kwao watu wasiokuwa na kazi mijini mwanzoni mwa miaka ya 80 ulifanya hali hii kuwa mbaya zaidi. Katika kipindi hiki, elimu ilikuwa na lengo la kuwaandaa watoto kwa maisha ya kutegemea kilimo. Jambo hili liliwafanya wasijiandae kwa ajili ya kufanya kazi viwandani na mjini maeneo ambayo ni muhimu kwa mageuzi ya kiuchumi. Zaidi ya hayo, utaifishaji uliwatisha wawekezaji na viwanda vilionekana kuwa ni vidogovidogo, hivyo kuwa na mchango mdogo sana kwa ukuaji wa uchumi na utengenezaji wa fursa za ajira. Sera

ya uchumi ambayo ilikuwa na lengo zuri lakini haikuwa na manufaa kutokana na kukumbwa na migogoro mingine duniani na vita vya Uganda, iliiacha Tanzania ikiwa na hali mbaya mwanzoni mwa miaka ya 80: nchi ilikabiliwa na viwango vya chini kabisa vya pato la taifa na ilikosa bidhaa muhimu, fedha za kigeni pamoja na misaada. Kwa ufupi, kiwango cha maendeleo ya binadamu nchini Tanzania kilikuwa na hali mbaya.

Kipindi kikuu cha pili cha Tanzania, kutoka 1986 hadi 2000, kilitawaliwa na ulegezaji masharti ya kibiashara na kuimarika kwa uchumi mkubwa. Ikichagizwa na mgogoro wa kiuchumi na kung'atuka kwa Nyerere, serikali ya Tanzania ilikubaliana na shinikizo kutoka kwa vyombo vya fedha vya kimataifa na kutekeleza mipango ya mabadiliko ya muundo wa kiuchumi. Mabadiliko hayo yalijumuisha kupunguza thamani ya shilingi ya Tanzania, kulegeza masharti ya soko la mazao na biashara, kuondoa ruzuku kwa wakulima, kusitisha utoaji wa huduma bure, kubinafsisha mashirika ya umma, na kupunguza ajira katika sekta ya umma na mishahara. Kwa ufupi, hali "ilirejeshwa nyuma" pale ilipowezekana. Matokeo ya mabadiliko hayo yalikuwa na madhara makubwa kwa maendeleo ya binadamu, hususan, kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi. Mafanikio madogo katika afya, elimu na kipato yaliyopatikana wakati wa ujamaa yalirudi nyuma. Uzalishaji katika kilimo ulipungua kwa sababu wakulima hawakuweza kununua mbolea kutokana na umasikini. Kutokana na kuanzishwa kwa uchangiaji gharama, utoaji wa huduma za jamii ambazo ni mhimili wa maendeleo ya binadamu, kama vile elimu na afya ulikabiliwa na hali mbaya. Zaidi ya hayo, nafasi nyingi za ajira zilipotea kutokana na kufumuliwa kwa mashirika ya umma. Rushwa iliongezeka sana kutokana na wafanyabiashara kutafuta vyeo katika ofisi za umma, na wale waliokuwa ofisini kuanza kutafuta miradi ya kibiashara. Ingawa uchumi hatimaye uliimarika, kiwango cha maendeleo ya binadamu kilishuka.

Kama nchi nyingi zinazoendelea, sera ya uchumi ya Tanzania katika kuingia karne mpya imekuwa na lengo kuu la kuondoa umasikini. Kimsingi, shughuli yote hii ilisukumwa na lengo kuu la jumuiya nzima ya wadau wa maendeleo kupitia dira za maendeleo kama vile Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Jitihada za Kupunguza Madeni za Taasisi za Bretton Woods, chini ya ufadhili wa Nchi Maskini Zenye Madeni Makubwa (HIPC). Kwa lengo hili la kuondoa umaskini, Tanzania iliandaa na kutekeleza mfululizo wa mikakati ya kupunguza umaskini (2001–2003); Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, yaani, MKUKUTA (2005–2010); na MKUKUTA wa pili (2010–2015). Wakati MKUKUTA umefikia lengo lake la kuimarisha ukuaji wa uchumi nchini Tanzania bado kuna changamoto katika kuondoa umaskini. Tanzania pia ina Dira ya Maendeleo ya Muda Mrefu ya 2025 iliyoandaliwa mwaka 2000. Dira hii inalenga kwamba hadi kufikia 2025, Tanzania iwe nchi yenye uchumi wa kati, ambao unadhihirishwa na amani, utawala bora, hali nzuri katika kujikimu, jamii ya watu wenye afya, kipato na elimu ya kutosha, pamoja na viwanda vya kati na uchumi wenye ushindani. Ili kufikia Dira ya Maendeleo ya 2025, serikali iliandaa mipango kadhaa ya muda mrefu, na ya muda wa kati, katika muundo wa Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano. Kulingana na mipango hii, maendeleo ya Tanzania yanapaswa kupitia katika hatua tatu. Katika hatua ya kwanza (mpango wa kwanza wa miaka mitano) kuanzia 2011 hadi 2016 vikwazo vikuu kwa Tanzania vilitakiwa kushughulikiwa. Kiuhalisia, hivi vilihusu vikwazo vikuu vya miundombinu – hasa nishati, bandari, barabara kuu na reli – pamoja na vikwazo vinavyohusiana na kukosekana kwa wafanyakazi wenye ujuzi, sayansi, teknolojia na ubunifu, teknolojia ya habari na mawasiliano, mazingira ya biashara kwa jumla na tija kwenye kilimo. Mpango wa pili wa miaka mitano, kuanzia 2016 hadi 2021, kimsingi utajikita katika kukuza ajira na kuongeza mapato kutokana na sekta ya viwanda, hasa viwanda vinavyohusiana na gesi asilia/mafuta, vya kusindika mazao ya kilimo na vinavyotumia teknolojia ya kati. Hatimaye, mpango wa tatu wa miaka mitano, kuanzia 2021 hadi 2026, utazingatia zaidi kuimarisha ushindani katika sekta zote, msisitizo mkubwa ukiwa kwenye viwanda na utoaji huduma. Kupitia ukuaji unaolenga kukuza mauzo ya nje, serikali inatarajia kuibadilisha Tanzania kuwa kitovu cha viwanda cha Afrika Mashariki.

## Masuala muhimu na Vikwazo katika utekelezaji wa Sera za Uchumi

Kupanga sera za kiuchumi na kuzitekeleza ni kazi mbili tofauti. Vipo vikwazo vya kufikia malengo ya sera na changamoto za kiuongozi ambazo zinatakiwa kuzingatiwa kadiri Tanzania inavyoendelea kutekeleza mchakato wa mageuzi ya kiuchumi ili yalete maendeleo ya binadamu.

Moja ya changamoto kubwa ambayo nchi nyingi zinazoendelea zinakabiliana nayo katika michakato yake ya maendeleo ni kuwa na uwiano sahihi kati ya ukuaji wa uchumi na maendeleo bora ya binadamu. Kuna vikwazo vitatu vinavyozuia njia ya kuwianisha mabadiliko ya kijamii na ya kiuchumi. Kwanza, kwa vile fedha na rasilimali zingine ni

chache na zinahitajika ili kuwezesha kusonga mbele kwa maendeleo ya binadamu, wakati wote ukuaji wa kiuchumi utajitokeza zaidi kuliko maendeleo ya binadamu. Hivyo, jambo muhimu ni kwamba uongozi wa nchi unajizatiti kuufanya uchumi upitie njia ya ukuaji unaowajali maskini kwa kutumia hatua za kisera zilizorekebishwa na ambazo zinaweza kufuatiliwa kwa karibu kwa kutumia viashiria na malengo yaliyowekwa. Pili, uboreshaji wa maendeleo ya binadamu unakabiliwa na hatari ya kuonekana tu kama utaratibu wa kuhimiza ukuaji wa uchumi. Matokeo yake, hatua za kisera zinaweza kulenga zaidi elimu ya kati, badala ya elimu ya msingi au utoaji huduma za afya, ambavyo vinaweza kuwa na mchango mkubwa zaidi katika kuondoa umaskini.

Licha ya masuala ya jumla yanayohusiana na kutafuta uwiano sahihi katika mageuzi ya kiuchumi, vikwazo vingine vitano vinatishia kuzuia kuyafikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2025. Kwanza, yapo mapungufu makubwa katika usimamizi wa sera, kama vile matatizo ya ukubalifu wa sera, ukosefu wa utaratibu wa kufuatilia na kufanya tathimini na mifumo ya kutoa mwongozo wa jumla, na mifumo na mikakati dhaifu ya mawasiliano serikalini. Kwa ulinganisho, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID) limebainisha vikwazo kadhaa vya nyongeza: ukosefu wa maelezo ya utendaji katika mipango na sera katika ngazi zote, katika utoaji vipaumbele, katika vyombo vya kufuatilia utimizaji wa majukumu na utendaji, pamoja na ukosefu wa uwajibikaji. Pili, vikwazo hivi vinazidishwa zaidi na ukweli kwamba Tanzania inakosa itikadi dhahiri ya kimaendeleo, kama vile ujamaa. Matokeo yake, sera na mipango inaweza kutafsiriwa kwa namna tofauti na wale wanaotakiwa kuitekeleza. Kikwazo cha tatu ni kwamba wale wanaotakiwa kusaidia katika utekelezaji – viongozi wa umma – vilevile, wanakabiliwa na vikwazo vikubwa. Licha ya mageuzi mengi katika miaka ya hivi karibuni, kuna mashaka makubwa kuhusu weledi na uadilifu wa watawala. Suala la nne ni kwamba Tanzania inakosa vyombo vya udhibiti, ambavyo ni wakala wa serikali, vinavyoweza kushughulikia mambo yanayosababisha ulegezaji wa masharti ya kibiashara kama vile kuwapo kwa bidhaa bandia na za kughushi, bidhaa za chini ya viwango zinazoingizwa ndani ya nchi, upangaji wa bei kubwa, au uharibifu wa mazingira. Yote haya yanawaumiza masikini kwa kiwango kikubwa. Hatimaye, Tanzania imeshindwa kufikia viwango vya ugatuaji wa madaraka. Hili ni tatizo kwa sababu ugatuaji wa madaraka ni muhimu katika kuchochea maendeleo katika maeneo mbalimbali: unaimarisha unyumbufu katika utekelezaji wa mipango, ufanisi katika utendaji wa serikali kwa vile unafupisha urasimu katika ufanyaji maamuzi, na uratibu katika ngazi ambazo madaraka yamegatuliwa. Katika kuhitimisha sehemu hii, Tanzania imeshuhudia na kutekeleza mtiririko mkubwa wa sera za kiuchumi tangu ilipopata uhuru wake. Kwa wastani, matokeo yake kwa maendeleo ya binadamu yamekuwa ya kukatisha tamaa. Ingawa kwenye karatasi mipango ya serikali kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi inaonyesha matumaini, hakuna uhakika kuwa itaweza kuitekeleza kwa ufanisi kutokana na vikwazo vikubwa vilivyopo. Sehemu inayofuata inatoa mwongozo zaidi wa namna ya kuufanya uchumi wa Tanzania ulete maendeleo ya binadamu.

# 4.

# Kuyafanya mageuzi ya kiuchumi yalete maendeleo ya binadamu nchini Tanzania

Sehemu zilizopita, katika ripoti hii, zimezungumzia hali ya maendeleo ya binadamu nchini Tanzania, namna mageuzi ya kiuchumi yanavyotokea na sera zipi za kiuchumi zimesababisha kutokea kwake. Sehemu hizo, zimebainisha kwamba licha ya kuwapo kwa maendeleo kwa kiwango fulani, ukuaji na mageuzi ya kiuchumi havijaonekana kuboresha maendeleo ya binadamu kwa kiwango cha kuridhisha. Sehemu inayofuata inalenga zaidi namna ya kuyafanya mageuzi ya kiuchumi yalete maendeleo ya binadamu nchini Tanzania. Kwa kuzingatia maudhui ya sehemu tatu zilizotangulia, sehemu hii inapendekeza na kubainisha sekta muhimu zaidi na vichocheo vya ukuaji vinavyotakiwa ili kuwa na mageuzi ya kiuchumi yenye mafanikio. Katika hatua ya pili, ripoti inajadili namna na aina za sera, mikakati, mipango na mifumo ya utekelezaji vinavyoweza kuhakikisha kwamba sekta hizi na vichocheo vya ukuaji kweli vinatekelezwa ili kuyafanya mageuzi ya kiuchumi yalete maendeleo ya binadamu.

## Mageuzi Muhimu ya Kiuchumi

Uchumi wa Tanzania unahitaji zaidi ya ukuaji ili kwenda katika mwelekeo sahihi. Zaidi ya kuongezeka kwa uzalishaji pekee, umuhimu pia upo katika kujumuisha ubora wa sifa za uzalishaji za kiuchumi zinazobadilika ambazo hutokea katika mchakato wa ukuaji wa uchumi. Tanzania inahitaji ukuaji unaotokana na uzalishaji katika sekta mbalimbali, iwe inayofanya uuzaji wa nje wenye ushindani, inayoongeza uzalishaji katika kilimo (ambapo watu wengi wanakitegemea ili kujikimu), katika makampuni, na ofisi/utendaji wa serikali, na inayotumia teknolojia iliyoboreshwa katika maeneo yote ya uchumi. Masuala haya yatakuza ukuaji jumuishi, ambao unatakiwa ili kuboresha maendeleo ya binadamu na ustawi wao.

Ili kutosheleza hitaji hilo, kunahitajika mikakati mahususi itakayoingilia kati. Kama ilivyoelezwa kwa undani katika sura ya pili ya ripori kuu, kutengeneza fursa za ajira zenye tija ni kiini katika kuufanya ukuaji wa uchumi uwe jumuishi zaidi, na hivyo, kupunguza umaskini na utofauti wa kipato. Hata hivyo, mpaka sasa, mageuzi ya kiuchumi yameshindwa kutengeneza ajira zenye malipo mazuri na tija kwa Watanzania wengi. Matokeo yake, nguvu kazi ya ziada imeishia kwenye sekta isiyo rasmi ambayo ina tija na malipo kidogo. Ili kuyafanya mageuzi ya kiuchumi yalete maendeleo ya binadamu, sera za serikali kuhusu ajira lazima zilenge kuongeza tija katika sekta zote. Sera na mikakati lazima ilenge kwenye utoaji huduma, hususan kwa kutilia mkazo ukuaji wa uzalishaji katika sekta muhimu za ukuaji ambazo ukuaji wake una athari kubwa zaidi katika kutengeneza ajira. Ripoti hii inataja sekta tatu muhimu ambazo ni viwanda, kilimo na utalii. Ukuaji wa uzalishaji katika sekta ya viwanda, kihistoria, sio tu umehusishwa na kutengeneza fursa nyingi za ajira; vilevile, umeweza kugusa sekta zingine kupitia uhusiano kati ya sekta zinazotoa malighafi na zile zinazopelekewa.

Kuongeza kiwango cha uzalishaji katika kilimo ni muhimu sana kwa sababu mbili. Kwanza, kilimo kinatoa ajira za moja kwa moja kwa takribani asilimia 80 ya watu wote; hivyo, kuongeza uzalishaji katika kilimo kutaleta matokeo ya haraka katika kupunguza umasikini na kuongeza ajira nchini Tanzania. Pili, kuongeza uzalishaji katika kilimo, kutasaidia kuchochea ukuaji, hasusan, kwa kusaidia sekta ya viwanda. Bila shaka, kwa kuzingatia uzoefu kuhusu maendeleo ya viwanda**,** kuongezeka kwa uzalishaji katika kilimo, kunawezesha kilimo kuchangia nguvu kazi katika viwanda na sekta nyingine zisizo za kilimo. Pia, kutasaidia kuzalisha chakula zaidi ili kuondoa migogoro kuhusu upandishaji wa mishahara katika viwanda vya mijini na kutoa mali ghafi kwa ajili ya usindikaji. Pamoja na hayo, kutaongeza uuzaji bidhaa nje ili kulipia mahitaji ya kufanyia mageuzi ya kilimo, na kuimarisha soko la ndani kwa ajili ya bidhaa za viwandani. Hata hivyo, ili kuongeza uzalishaji, serikali ya Tanzania lazima iondoe vikwazo na kutoa uhuru mkubwa kwa wazalishaji. Inatakiwa kuwezesha upatikanaji wa pembejeo za kilimo na teknolojia inayowezesha uzalishaji, kuboresha mzunguko wa thamani ya mazao,[7] na mifumo fanisi ya masoko inayohusianisha vema na sekta ya viwanda, na kuhamasisha matumizi makubwa zaidi ya kilimo cha umwagiliaji. Nchini Tanzania, kati ya hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, ni hekta milioni 0.39 tu, kwa sasa, zinazomwagiliwa. Zaidi ya hayo, ni muhimu kwa Tanzania kutumia fursa yake kulinganisha biashara ya kilimo na ile ya mazao yaliyochakatuliwa

7 Value chain


viwandani. Biashara zote mbili zina uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira na kuingiza kipato. Uchakatuaji wa mazao viwandani kwa namna ya pekee unaimarisha sekta zinazotoa malighafi na zile zinazopelekewa bidhaa katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

Utalii ni sekta ya tatu muhimu iliyobainishwa na ripoti hii, kwa sababu kuu tatu. Kwanza, Tanzania inayo fursa linganifu na shindanifu katika sekta hii kutokana kujaliwa maliasili za wanyama na mimea ambazo hazijaharibiwa, mazingira asilia yanayopendeza, mazingira mazuri kwa wasafiri na serikali yenye kusaidia ambayo inatambua haja ya kuwepo uongozi wa sekta binafsi. Pili, sekta hii inahitaji nguvu kazi kubwa, inayomaanisha kwamba ukuaji wake utawanufaisha watu wengi zaidi na utachangia kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa baada ya muda fulani. Mwisho, inachochea ukuaji katika sekta zingine kutokana na mahitaji makubwa ya mazao ya sekta hizo, kama vile chakula, bidhaa za viwandani, maua, kazi za mikono na burudani. Licha ya kuongeza fursa za ajira kwa njia ya kupanua sekta ya kilimo, kuendeleza viwanda na kupanua utoaji huduma, yapo mambo manne zaidi ya kimkakati yanayoweza kusaidia kama kiini cha kuhusianisha ukuaji wa kiuchumi na maendeleo ya binadamu. Kwanza, ni kuongeza ukuaji wa mauzo ya nje. Miongoni mwa mambo mengine, kuuza bidhaa au mazao nje kunatoa fursa ya kupanua uzalishaji, kutumia fursa ya kulinganisha sekta mbalimbali, na kuongeza tija na kukuza uchumi kupitia ushindani. Matokeo yake, ni kuongeza ajira, kipato na ujuzi, na hatimaye, kuchochea ukuaji wa viwanda.

Kama iliyoelezwa kwa kina katika sura ya pili ya ripoti kuu, mafanikio ya mageuzi ya kiuchumi yanategemea michakato miwili ya kuongeza fursa za ajira na upanuzi mkubwa wa huduma za jamii kama elimu na afya. Sekta hizi zinatumia nguvu kazi kubwa, hivyo, kuwa na uwezo mkubwa wa kuongeza fursa za ajira. Pia, zinapeleka kwenye uchumi nguvu kazi yenye afya bora na iliyoelimika vema, ambayo inatakiwa ili kuustawisha uchumi. Hata hivyo, elimu na afya zinabakia kuwa moja ya vikwazo vya ukuaji jumuishi wa kiuchumi. Ili kufikia viwango toshelevu vya utoaji wa huduma hizi hadi mwaka 2025, zaidi ya walimu 900,000 wenye sifa stahiki lazima waajiriwe, na ajira katika sekta ya afya italazimika kuzidishwa mara nne. Zaidi ya hayo, uwekezaji katika taasisi bora za afya na shule unatakiwa sana. Inayohusiana kwa karibu sana ni hatua ya tatu: yaani kukuza mtaji wa rasilimali watu na kujenga ujuzi. Kulingana na maendeleo ya sasa ya kidemografia (tazama Kielelezo cha 7), Tanzania inao uwezo wa kuifikia “faida ya kidemografia”[8] katika miaka thelathini hadi arobaini ijayo. Hii ina maana kuwa idadi ya wazalishaji itazidi idadi ya watumiaji au walaji. Hata hivyo, ili kuifikia faida hii ya kidemografia, serikali lazima ihakikishe kwamba wazalishaji hawa kwa kweli wanazalisha, yaani wanapata ajira. Hili litawezekana tu iwapo elimu itatoa nguvu kazi yenye ujuzi mwafaka unaoweza kutumiwa kwenye masoko shindani ya ndani na ya kimataifa, na kiubunifu kuwashirikisha Watanzania katika shughuli za ujasiriamali na kujiajiri.

## Kielelezo cha 7

Kiwango cha ongezeko la watu wanaofanya na wasiofanya kazi




Chanzo: Agwanda na Amani, imekokotolewa kutoka Kitengo cha Idadi ya Watu cha Idara ya Uchumi na Masuala ya Kijamii ya Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa, Matarajio ya Idadi ya Watu Duniani: Pitio la 2012, http://esa.un.org/unpd/wpp/index.htm.

8 Demographic dividend

Mwisho, kufungua fursa na uwezo wa sekta zilizobainishwa za ukuaji kuna ulazima wa kuwekeza sana katika miundombinu ya usafirishaji na nishati. Kupanua sekta ya usafirishaji kuna matokeo kadhaa ya moja kwa moja katika ukuaji jumuishi wa kiuchumi: kunatengeneza fursa za ajira, kunaokoa muda na gharama, kunawezesha upatikanaji wa masoko na ushindani katika biashara, na huongeza uwekezaji kutoka nje. Pamoja na hayo, kufungua sekta ya usafirishaji kunaambatana na athari ambazo sio za moja kwa moja. Kunawezesha uzalishaji wa bidhaa anuai, uzalishaji wa kiwango kikubwa na faida ya gharama za bidhaa[9] kutokana na upatikanaji mkubwa wa soko. Vilevile kunawezesha kuunganisha sekta mbalimbali; kuongeza tija na thamani kutokana na upatikanaji wa pembejeo bora na ushindani mkubwa. Kwa jumla, kunashusha bei za bidhaa na huduma na kunafanya ziwe anuai; hatimaye, kunawezesha utoaji wa huduma za jamii. Vivyo hivyo, nishati ni hitaji muhimu sana ili kupata mageuzi ya kiuchumi yenye mafanikio. Ni rasilimali muhimu sana kwa sekta zote za uchumi, hasa zile za uzalishaji zaidi, na ni muhimu sana katika kuboresha viwango vya maisha na kuleta maendeleo ya binadamu.

## Mambo Muhimu katika Kuhakikisha Uhusiano Wenye Manufaa kati ya Mageuzi ya Kiuchumi na Maendeleo ya Binadamu

Mageuzi ya kiuchumi kwa ajili ya maendeleo ya binadamu hayatokei yenyewe. Yanahitaji usimamizi na mwongozo wa serikali katika maeneo manne. Kwanza, serikali inatakiwa kusimamia uchumi kwa umakini mkubwa, yaani kutekeleza sera za kifedha zenye manufaa kwa ajili ya kuongeza ukuaji wa haraka katika pato la ndani la taifa, ajira na mauzo ya nje; kuwianisha matumizi yake ya muda mfupi na uwekezaji wa muda mrefu; kufanya ununuzi wa umma uendane na fedha zilizotumika; kuondoa rushwa katika maeneo yote; kuongeza ufanisi wa viwanja vya ndege, bandari na vivuko vya mipakani kwa usimamizi wa karibu; kudhibiti kile tu kinachoweza na kinachopaswa kudhibitiwa; na hatimaye kuandaa kwa wakati na kwa ubora wa hali ya juu takwimu za kijamii na kiuchumi ili kuiwezesha kupanga mipango bora, kufuatilia utekelezaji na kubadili mwelekeo pale inapolazimu.

Pili, serikali inapaswa kushirikiana kwa ukaribu na sekta binafsi. Kwa upande mwingine, inapaswa kushauriana sana na sekta binafsi wakati wa kuandaa sera na mikakati na hususan, zile zinazolenga kutengeneza mazingira mazuri ya kibiashara. Kwa upande mwingine, serikali inapaswa kuendelea kuilea sekta binafsi kwa kutoa miundombinu na huduma saidizi, kuendeleza mazingira mazuri ya usimamizi wa shughuli za ujasiriamali, na kuzirahisisishia kampuni binafsi kupata teknolojia mpya na kuingia katika shughuli mpya za kiuchumi na masoko mapya. Mifano mizuri ya ushirikiano mkubwa na uliofanikiwa kati ya sekta za umma na bifasi inaweza kupatikana katika historia ya maendeleo ya nchi za Asia Mashariki. Zaidi ya hayo, ni muhimu kwamba serikali ijumuishe na kuhamasisha asasi za kiraia, ili iweze kuhakikisha kwamba ushirikiano wa karibu kati ya maofisa na asasi usaidie mageuzi ya kiuchumi.

Moja ya changamoto kubwa kabisa ambazo Tanzania inakabiliana nazo katika kufanikisha mageuzi ya kiuchumi kwa maendeleo ya binadamu ni uratibu ndani ya serikali ili kuandaa na kutekeleza sera kubalifu na halisi. Hili linaletwa na sababu kuu mbili. Kwanza, sera na mipango mara nyingi inatolewa na asasi za nje, hii ndiyo sababu ya umiliki na ari ya wafanyakazi wa serikali kuwa chini. Pili, kwa kuwa Tume ya Mipango inajitegemea, na haipo chini ya Wizara ya Fedha, ni mara chache huwa na ushawishi mkubwa katika kuhakikisha matumizi katika mipango yake yanawekwa kwenye bajeti kama yalivyo.

Hatimaye, majukumu muhimu ya msaada wa serikali ili kuleta mageuzi ya kiuchumi yanapaswa kutekelezwa kwa usahihi. Kwa hiyo, taasisi zinazosimamia majukumu haya na watu wanaofanya kazi katika taasisi hizo wanatakiwa wawe waadilifu. Taasisi hizi zinajumisha Benki Kuu, Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango ya Taifa, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Wizara ya Kukuza Uwekezaji na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kiongozi aliye makini katika kuchochea mageuzi ya kiuchumi, anapaswa kuteua wakuu wa kusimamia majukumu muhimu kwa kuzingatia umahiri na uwezo wa kuleta matokeo. Vivyo hivyo, inapaswa kuzingatiwa katika uteuzi wa wakurugenzi na manaibu wao katika wizara hizi.

9 Economies of scale

# UJUMBE MAHUSUSI

- **Ukuaji wa uchumi pekee hautoshi katika kuchochea maendeleo ya binadamu nchini Tanzania**
  Licha ya kuwa na viwango vya juu vya pato la taifa katika muongo uliopita, mafanikio katika kuondoa umasikini ni madogo sana. Tanzania bado ni miongoni mwa nchi zenye kiwango cha chini sana cha maendeleo ya binadamu duniani. Uzoefu uliopatikana Tanzania katika muongo uliopita, umeonyesha kutokuwapo kwa uwiano kati ya kukua kwa uchumi na kupungua kwa umasikini. Kwa hiyo, ripoti hii inapendekeza, kwa uwazi, kuchukuliwa kwa hatua mahususi kushughulikia ukuaji wa uchumi ili kupunguza umasikini.

- **Ili kuchochea maendeleo ya binadamu, Tanzania inahitaji kufanya mageuzi katika  uchumi wake**
  Siku hizi, nchi zote zinazofahamika kuwa za viwanda au zilizoendelea zimefuata mikondo inayofanana sana ya maendeleo ya kiuchumi: kwa kuacha kutegemea kilimo na kuelekea kwenye viwanda na huduma, pamoja na mabadiliko katika idadi ya watu kwa kuwa na viwango vya chini vya vizazi na vifo. Kwa kufuata njia hii ya mageuzi ya kiuchumi, Tanzania inahitajika kuboresha hali yake ya maendeleo ya binadamu.

- **Ili kuleta maendeleo ya binadamu, ukuaji na mageuzi ya kiuchumi vinapaswa kuongeza ajira na utoaji wa huduma za jamii**
  Uchumi wa Tanzania umebadilika kwa kiwango kidogo sana katika muongo uliopita: wakati mchango wa kilimo katika pato la taifa umepungua kidogo, ule wa sekta za viwanda na huduma umeongezeka kwa asilimia fulani. Hata hivyo, mageuzi haya ya kiuchumi, yasiyo ya kudumu, hayajaboresha viwango vya maisha ya wananchi walio wengi. Sababu ya hili ni kwamba ukuaji na mageuzi ya kiuchumi nchini Tanzania vimeshindwa kupanua fursa za ajira na kuboresha huduma za jamii. Utengenezaji wa fursa za kutosha za ajira na ujira mzuri ndivyo vinavyoweza kuleta ukuaji wa uchumi ulio jumuishi zaidi, na hivyo kupunguza umasikini na kuboresha maisha. Zaidi ya hayo, huduma bora za jamii huhakikisha sekta ya uchumi inapata nguvu kazi yenye afya njema na elimu bora kwa mahitaji yake.

- **Kilimo, viwanda na utalii ni sekta tatu muhimu za ukuaji ambazo Tanzania ni lazima izilenge zaidi.**
  Kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi ya haraka na jumuishi, Tanzania inahitaji kuongeza tija katika uchumi wake pamoja na fursa za ajira. Kutokana na kupanuka kwa uhusiano kati ya sekta zinazotoa malighafi na zile zinazopelekewa. ukubwa wa nguvu kazi, pamoja na uwezekano wake mkubwa wa kuongeza uzalishaji, sekta za kilimo, viwanda na utalii zinatarajiwa kufanya mageuzi ya kiuchumi  nchini Tanzania kwa manufaa ya watu wake.

- **Vikwazo katika miundombinu ya jamii na usafirishaji lazima viondolewe ili kuwezesha ukuaji katika sekta tatu muhimu**
  Bila ya kuwa na nguvu kazi iliyoelimika na yenye afya njema, uchumi wa Tanzania hauwezi kukua na kubadilika kwa namna inavyotakiwa ili kuleta maendeleo ya binadamu. Vilevile, miundombinu bora ya usafirishaji ni hitaji mojawapo ili kufikia lengo la kuongeza tija katika kilimo, viwanda na utoaji huduma. Miundombinu hiyo inasaidia kuyafikia masoko mapya, inawezesha uzalishaji mkubwa, inaunganisha sekta mbalimbali, inawezesha utoaji wa huduma za jamii, pia, inaokoa muda na gharama. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwa serikali kuongeza matumizi katika maeneo haya mawili.

- **Ili mabadiliko ya uchumi yawe na tija kwa maendeleo ya binadamu, Tanzania inahitaji uongozi uliojizatiti na bora unaofanyia kazi sera bora za uchumi**
  Mageuzi ya kiuchumi hayaonekani moja kwa moja katika maendeleo ya binadamu. Ili maendeleo ya binadamu yapatikane, kuna haja ya kufanya maamuzi ya makusudi ya kisera na kutekeleza mikakati inayoelekeza rasilimali kwenye sekta mahususi, na muhimu zaidi kwenye sekta za kijamii. Serikali inatakiwa kuchukua wajibu mkubwa katika hili, kwa kushauriana, kwa karibu zaidi na sekta binafsi na asasi za kiraia. Itatakiwa kutekeleza sera muhimu za kiuchumi na zinazojali maskini ambazo zinaongeza tija na fursa za ajira, husasan katika sekta tatu muhimu za ukuaji.

- **Serikali lazima ijenge uwezo wake wa kusimamia na kuratibu, ili kutekeleza, kwa mafanikio, sera za kiuchumi kwa ajili ya maendeleo ya binadamu.**
  Kuandaa na kutekeleza sera za kiuchumi sio kazi rahisi. Kazi zote mbili zinahitaji taasisi zenye watendaji bora, uratibu mzuri na zilizojizatiti kikamilifu. Tanzania bado inayo masuala mengi ya kufanya katika eneo hili. Kutokana na mifano yenye mafanikio ya nchi za Mashariki mwa Bara la Asia, hatua moja ya kwanza ingekuwa kuunda bodi ya mipango ya kiuchumi, ambayo chini ya uongozi wa moja kwa moja wa Rais au Waziri Mkuu huratibu wadau muhimu ndani ya serikali.

Empowered lives.
Resilient nations.

United Republic of Tanzania

ESRF
Implementing Partner

Katika zama hizi, maendeleo ya Tanzania yanachagizwa na mikakati mikubwa minne: yaani, Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025, Mpango wa Muda Mrefu wa 2011/12 – 2024/25, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2010/11 – 2015/16, na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania 2010/11 – 2014/15 (MKUKUTA II). Lengo hasa la mikakati hii ni kuhakikisha kwamba mpaka kufikia mwaka 2025, Tanzania inakuwa nchi ya kipato cha kati, ikiwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya binadamu na pato la mwaka la zaidi ya dola 3,000 za Marekani kwa kila mtanzania. Kielelezo kikuu cha maendeleo ya Tanzania katika kipindi hiki kitakuwa mageuzi ya kiuchumi kutoka uchumi unaotegemea kilimo chenye tija ndogo hadi uchumi wa kati unaotegemea viwanda, ukiambatana na sekta muhimu na inayokua kwa kasi ya huduma.

Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu nchini Tanzania ya 2014 ni toleo la kwanza. Mada kuu ya ripoti hii ni "Mageuzi ya Kiuchumi kwa Maendeleo ya Binadamu". Katika muongo uliopita, kumekuwa na mabadiliko katika mtazamo wa sera za maendeleo kutoka mtazamo unaojali kiwango (cha ukuaji wa jumla wa uchumi) na uzalishaji, na kuelekea kwenye kujali mabadiliko ya thamani ya ukuaji wa kiuchumi (unaomnufaisha mtu mmoja mmoja) kama inavyoonyeshwa kwenye dhana nzima ya mageuzi ya kiuchumi. Ripoti hii inachambua aina za mageuzi ya kiuchumi zinazotakiwa ili Tanzania iwe nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Zaidi ya hayo, ripoti hii inatoa uelewa mpana wa mwingiliano kati ya mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu nchini Tanzania, hasa changamoto, fursa na vikwazo vyake.

'Uhuru na maendeleo vina mahusiano kama wa kuku na mayai. Bila kuku huwezi kupata mayai na bila mayai baada ya muda mfupi hutakuwa na kuku. Vilevile, bila uhuru huwezi kupata maendeleo, na bila maendeleo baada ya muda mfupi sana unapoteza uhuru. Kwa hiyo, ukweli ni kwamba maendeleo yanamaanisha maendeleo ya watu: barabara, majengo, ongezeko la uzalishaji wa mazao n.k. sio maendeleo; bali ni zana tu kwa ajili ya maendeleo.'

\- Julius Nyerere, kutoka Sura ya 1

'Maendeleo yanaweza kuonekana kama mchakato wa kupanua uhuru halisi ambao watu hufurahia.'

\- Amartya Sen, kutoka Sura ya 1

'Kila pendekezo lazima liamriwe kwa kigezo cha iwapo linatimiza lengo la maendeleo na lengo la maendeleo ni watu.'

\- Julius Nyerere, kutoka Sura ya 3

www.thdr.or.tz